# Mtoto Jifunze

# Vitendawili, Methali, Vinyonga ulimi, Vipimo, Misemo na Hadithi



PAL NETWORK People's Action for Learning

ELTU Every Language Teaches Us

uwezo TANZANIA

## Utangulizi

Mtoto Jifunze, Vitendawili, Methali, Vinyonga ulimi, Vipimo, Misemo na Hadithi ni kitabu kwa ajili ya watoto wa darasa la kwanza na wengine wanaopenda kujifunza stadi za kusoma na lugha ya Kiswahili. Kitabu hiki ni kizuri kwa watoto kwa sababu kinawafundisha watoto namna ya kutega Vitendawili rahisi na kuvitegua, kinawafundisha methali za Kiswahili na maana zake na kinafundisha pia vipimo vinavyopatikana katika mazingira yao halisi. Vilevile, kinafundisha misemo inayopatikana katika mazingira yao ya kila siku pamoja na hadithi zinazowajengea ubunifu, ujasiliamali pamoja na bidii katika kazi.

Kitabu hiki kimeandaliwa na Shirika la Uwezo Tanzania, kwa ufadhili wa mtandao wa People's Action for Learning Network (PAL NETWORK) wenye makao yake makuu Jijini Nairobi,Kenya. Kitabu hiki ni matokeo ya utafiti kupitia mradi uliojulikana kwa jina la Every Language Teaches Us (ELTU) uliofanyika mwishoni mwa mwaka 2021 katika wilaya nne za Tanzania bara ambapo ulilenga kukusanya rasilimali lugha kutoka katika lugha za Kipare,Kisukuma,Kimasai na Kiswahili.

Rasilimali lugha zilizochapishwa katika kitabu hiki ni baadhi tu ya zile zilizokusanywa. Wazee kutoka wilaya za Mwanga, Ilemela, Arusha na Kisarawe walifikiwa na watafiti kutoka shirika la Uwezo Tanzania na waliweza kutaja rasilimali lugha hizi katika asili kabisa ya lugha zao, ambapo badae Uwezo ilitafsiri katika lugha ya Kiswahili na kuweza kuchapisha kitabu hiki, kwa lengo la kuwasaidia watoto kujifunza na kuinua umahiri wa kusoma.

Hairuhusiwi mtu yeyote kunakili au kuchapisha kitabu hiki bila idhini ya Shirika la UWEZO TANZANIA (TANZANIA) na PAL NETWORK (KENYA).

© Uwezo Tanzania
Toleo la Kwanza 2023
ISBN: 978-9912-9963-4-2

Uwezo Tanzania
S.L.P 8259
Dar es Salaam
Simu: +255 735 041 143
Baruapepe: info@uwezotanzania.or.tz
Tovuti: www.uwezotanzania.or.tz

## VITENDAWILI

1. Kitendawili? Tega!
   Watoto wangu wanamvisha Nakide nguo.
   Jibu: Kujenga nyumba



2. Kitendawili? Tega!
   Askari huku na kule lakini hawawezi kunichoma mkuki.
   Jibu: Meno na ulimi

3. Kitendawili? Tega!
   Mlinzi wetu haachi kwenda kazini.
   Jibu: Mlango

4 Kitendawili? Tega!
Mtoto wangu nikimpa chakula analia, nikimnyima halii.
Jibu: Redio na betri

5 Kitendawili? Tega!
Kijana wangu ni rasta.
Jibu: Muhindi



6 Kitendawili? Tega!
Ubwabwa wa mwana mtamu.
Jibu: Usingizi



7 Kitendawili? Tega!
Bibi mweupe ametupwa mibani.
Jibu: Machicha ya nazi

8 Kitendawili? Tega!
Mwiba wa tumboni unauma
Jibu: Njaa

## METHALI

1. Methali? Methali!
Damu nzito kuliko maji.
Maana: Ndugu yako ni wa muhimu sana; mjali na umpende



2. Methali? Methali!
Baada ya dhiki faraja.
Maana: Kila wakati mgumu ambao mtu anaupitia, utaisha na utakuja wakati wa raha.

3. Methali? Methali!
Haba na haba hujaza kibaba.
Maana: Ukikusanya kidogo kidogo baadae hukamilika na kuwa kitu kizima.

4. Methali? Methali!
Mkono mtupu haulambwi.
Maana: Watu wasio na utajiri wa mali au fedha wanadharauliwa na hawana mvuto wa kuwa na marafiki wengi wala kuheshimiwa katika jamii.  kwa hiyo, fanya kazi kwa bidii.

5 Methali? Methali!

Mgaa gaa na upwa hali wali mkavu.

Maana: Anayejishughulisha hakosi kupata chochote.

6 Methali? Methali!

Kusikia kwa kenge mpaka damu itoke masikioni.

Maana: Kumwadhibu mtu ambaye sio msikivu ni vigumu kuelewa hadi madhara yatakapompata.



7 Methali? Methali!

Asiyesikia la mkuu huvunjika guu.

Maana: Mtu asiyesikiliza nasaha za wazazi au wazee huishia kukosa mafanikio ama kuumia

8 Methali? Methali!

Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

Maana: Asiyesikiliza ushauri kutoka kwa wazazi wake atakumbana na matatizo  ya ulimwengu na mwisho wake huwa ni mbaya.

9 Methali? Methali!

Joto la jiwe analijua mjusi.


Maana: Uhalisia wa jambo analijua mhusika

10 Methali? Methali!

Mbwa hushikwa shingo na anayemfuga.

Maana: Siku zote binadamu humtii na kumpenda anayemjali

11 Methali? Methali!
Mifugo iliyopelekwa mtoni hailazimishwi kunywa maji.
Maana: Ukishamuonesha mtu njia ya mafanikio, ni jukumu lake kukubali na kufuata au kukataa na kutofuata.



12 Methali? Methali!
Akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli.
Maana: Anayekusaidia wakati wa shida ndiye rafiki wa kweli.

13 Methali? Methali!
Anayejua maumivu ya kidole ni ukucha.
Maana: Anayejua maumivu yako ni yule anayekujali au aliye karibu nawe.

## VINYONGA ULIMI

***Lengo: kufanya mazoezi ya matamshi***

1. Mpishi mbishi kapika ubwabwa mbichi.




2. Kaka, kale kakuku kangu kadogo-kadogo kako kwako kaka?
3. Kaanzia Kimanzichana, kapitia Manzese, Sinza kwa Mzanzibari na kamaliz-ia (safari) Chalinze kwenye mazishi.
4. Pita akasita, akaita, 'Tarita', akapita na kukita Gitaa juu ya mita (ya maji).
5. Katibu kata wa kata ya Mkata kawakataza kata-kata wakazi wa Kata ya Mkata kukata-kata miti katika Kata ya Mkata.
6. Tupe tupate tumtupie tapu.
7. Nina wamnunia nani, nunu naye kesha nuna?
8. Kikujiacho kitakachokuondoka.
9. Hapo ulipo tupo hapo.
10. Twanga tope nitwange tope, tope hilo latwangwaje?
11. Nimenufaika kutunukiwa tunu na nunu.
12. Karimu ni mkarimu na ana karama.
13. Mbuzi hali nazi kwa vile hawezi kupanda ngazi, ndipo azifikie nazi.
14. Wale wali wa liwali wale wali wa liwali.
15. Kipi kikusikitishacho?

## VIPIMO

1. Mwalimu: - Vipimo? Vipimo!
   Wanafunzi: Vipimo!
   Hatua za miguu
   Kipimo cha kupimia ukubwa wa ardhi au eneo. Mfano: Shamba au Kiwanja.



2. Kamba
   Inatumika kupimia urefu wa vitu: mfano unaweza kupima, urefu wa shamba, chumba na vitu mbalimbali.
3. Sado moja
   Chombo kinachotumika kupima vitu katika ujazo ulio sawa na kilo 4.
4. Debe au ndoo kubwa
   Chombo kinachotumika kupima ujazo wa vitu ulio sawa na kilo 20 au lita 20.
5. Gunia moja
   Mfuko ambao mara nyingi hutumika kuhifadhia nafaka. Kwa kawaida unabeba ujazo wa debe 5-6, sawasawa na ujazo wa kilo 100 hadi120.
6. Kibaba/lita/Kimbo
   Chombo cha kupimia vitu kwenye ujazo wa lita 1.



## MANENO YA HEKIMA (KANUNI)


1. Mwalimu: Misemo? Misemo!
   Wanafunzi: Misemo!
   Asiyelalamika hakombolewi.
   Maana: anayeficha matatizo hawezi kupata msaada.

2. Mwalimu: Misemo? Misemo!
   Wanafunzi: Misemo!
   Mpenda uzuri hukatika sikio.
   Maana: Kupata urembo sharti udhurike, au Ili mtu afanikiwe lazima apitie maumivu na awe mvumilivu.

3. Mwalimu: Misemo? Misemo!
   Wanafunzi: Misemo!
   Usikatae wito kataa maneno.
   Maana: Usikatae unachoitiwa. Sikiliza kwanza ndio utoe maamuzi.

4. Mwalimu: Misemo? Misemo!
   Wanafunzi: Misemo!
   Afadhali jeshi la kondoo linaloongozwa na simba kuliko jeshi la simba linaloongozwa na kondoo.
   Maana: Ni vizuri kuwa na kiongozi imara, mwenye maono anayeweza akaongoza wafuasi dhaifu, kuliko kuwa na wafuasi imara, wenye maono wanaoongozwa na kiongozi dhaifu.

5. Mwalimu: Misemo? Misemo!
   Wanafunzi: Misemo!
   Usihesabu vifaranga kabla kuku hajaangua mayai.
   Maana: Usisherehekee ushindi kabla jambo halijafika mwisho/ halijakamilika.
   Ni vigumu kujihakikishia hitimisho la baadhi ya mambo fulani, mpaka hatua fulani ya lazima ifike kwanza.



6 Mwalimu: Misemo? Misemo!

Wanafunzi: Misemo!

Huwezi kumfundisha mbwa mzee mbinu mpya za uwindaji.


Maana: Wazee wamezoea kufanya mambo kwa mtindo fulani, tofauti na mitindo ya kisasa inayoambatana na matumizi ya zana za kisasa.

7 Mwalimu: Misemo? Misemo!

Wanafunzi: Misemo!

Ulimi ni mkali kuliko jambia.

Maana: Matumizi mabaya ya maneno yanaweza kuleta madhara makubwa kwa watu.



## MISEMO

1. Shingo haizidi kichwa.

   Maana: Mdogo hawezi kumzidi mkubwa kwa uzoefu au hekima. Hivyo ni muhimu kuwaheshimu watu waliokuzidi umri/ wakubwa.

2. Pembe ni Akili.

   Maana: Utafutaji unahitaji kutumia akili ili kuleta matokeo chanya.

3. Mfinye sikio.

   Maana: Mwambie mtu jambo fulani lililofichika asilolijua ili alijue. Mfano. Kumuokoa asiibiwe, asikosee.n.k.

## HADITHI FUPI

### 1 Mwamba Apambana na Jitu

Hapo zamani za kale, katika nchi ya Usukumani, alikuwepo jitu mla watu. Jitu huyo aliitwa Shing'weng'we. Pia, alikuwepo bibi aliyeitwa Kabula. Bibi Kabula alikuwa na kijana aliyeitwa Mwamba. Bibi Kabula alimfundisha Mwamba ujasiri. Mwamba alianza kutengeneza mishale imara sana. Alikuwa akiimba: "Shing'weng'we, Shing'weng'we kawameza watu × 2.

Mwamba alipokuwa kijana mkubwa, alibeba mishale yake. Alienda kulisaka jitu msituni kote. Alipoliona, alilirushia mshale na ukalichoma kifuani. Jitu lilianguka chini na kufa palepale. Mwamba alirudi kijijini kwa furaha huku akiimba wimbo wa ushindi. Wimbo huo ulikuwa wa nimemuua Shing'weng'we, aliyemaliza ndugu zangu. Wanakijiji waliposikia wimbo, walitoka kumlaki kwa shangwe. Tangu siku hiyo, watu wote walimwita Mwamba shujaa wa Usukumani.

**Fundisho:**

Tuwafundishe watoto tangu wakiwa wadogo kujiwekea malengo katika maisha, kufanya kazi za fani mbalimbali na kuwajengea stadi za ujasiri wa kupambana na maadui katika mazingira wanayoishi.




## Marafiki

2 Hapo zamani za kale, katika nchi ya mbali, kulikuwa na marafiki wawili. Mmoja aliitwa Nanga na mwingine aliitwa Sayayi. Nanga alikuwa mkarimu na Sayayi alikuwa mchoyo.

Siku moja walienda kutafuta chakula shambani. Walipokipata, walikileta nyumbani ili kiliwe pamoja. Walipokifikisha tu nyumbani, Sayayi alimwambia Nanga kuwa anaitwa na mjomba wake. Nanga alienda kwa mjomba wake. Sayayi alikula chakula chote! Nanga aliporudi, alikuta chakula chote kimeliwa. Alimuuliza Sayayi lakini Sayayi alimsingizia mbwa wao. Siku nyingine tena walienda kutafuta chakula porini. Walipokipata, walikileta nyumbani. Sayayi alimwambia tena Nanga kuwa anaitwa na shangazi yake. Nanga alimwambia Sayayi kuwa waende wote. Sayayi alikubali. Wote walianza safari. Walipofika njiani, Sayayi alimwambia Nanga kuwa anarudi kwanza nyumbani. Nanga aliendelea na safari. Sayayi alipofika nyumbani, hakukuta chakula chochote. Sayayi alianza kujuta kwa kitendo chake cha uchoyo. Aliamua kumwomba rafiki yake msamaha. Nanga alimsamehe. Sayayi aliacha tabia ya uchoyo. Wote waliendelea kutafuta chakula na kula kwa pamoja.

### Fundisho:

1. Uchoyo, ubinafsi na uongo huua urafiki.
2. Mtambue mapema rafiki mwenye hila na dhuluma.



## 3 Mzee wa Hekima

Hapo zamani za kale, katika kijiji kimoja, kulikuwa na mzee mmoja tajiri sana. Mzee huyo alikuwa na hekima. Alipenda sana kusimulia hadithi kwa mifano. Mifano yake ilikuwa na mafundisho mazuri kuhusu maisha. Mzee huyo alikuwa na watoto watatu. Alipenda sana watoto wake waishi kwa umoja ili wafanikiwe.

Siku moja aliwaita watotot wake wote. Aliwapa kila mmoja vijiti vitatu ili avivunje vikiwa pamoja. Kila mmoja alishindwa. Hatimaye aliwaambia wote kwa pamoja wavunje vijiti hivyo, Walifanikiwa kuvivunja vijiti hivyo kwa urahisi sana. Mzee aliwaambia kuwa wakishikamana wote, hakuna adui atakayewashinda.

### Fundisho:

Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu. Mkishirikiana kila jambo kwenye maisha mtafanikiwa.



## 4 Miraa na Lemba waenda kumchumbia Nashivai

Hapo zamani za kale, katika kijiji cha Olmotonyi aliishi Mzee Moleli. Mzee huyu alikuwa na binti yake aliyeitwa Nashivai. Siku moja Miraa na Lemba walienda kumchumbia Nashivai. Mzee Moleli alitaka kijana wa kumchumbia binti yake awe anayeweza kuchunga mifugo ikashiba vizuri. Aliamua kuwapima uwezo vijana hao.

Siku ya kwanza, alimkabidhi Miraa mifugo ili akawachunge. Miraa aliwapitisha mifugo kwenye nyasi nyingi. Walikula vya kutosha wakashiba. Waliporudi wote walilala na kutulia.

Siku ya pili, Lemba alikabidhiwa mifugo akawachunge. Aliwapitisha kwenye majani makavu ya miti. Walikula kwa tabu na hawakushiba kabisa. Waliporudi, hawakulala hata kidogo bali walisumbua sana. Hivyo, walianza kula majani mabichi ya miti ya uzio. Mzee Moleli alikasirika sana na hakulidhishwa na utendaji kazi wa Lemba. Aliridhishwa pasipo shaka na utendaji kazi wa Miraa. Kwa hiyo, alimkubalia Miraa amchumbie binti yake, Nashivai.

**Fundisho:**

Utafutapo jambo, lifanyie kazi kwa bidii na maarifa.



## 5 Kinyonga Mjanja

Hapo zamani za kale, Sungura na Kinyonga ambao walikuwa marafiki waliishi msituni. Walimwona msichana mzuri sana akikatiza msituni. Msichana huyo aliitwa Marisa, binti wa Mzee Kobe. Sungura na Kinyonga walitamani kumuoa Marisa. Wote walianza kugombania msichana huyo. Kila mmoja aliamua kupeleka posa kwa Mzee Kobe. Mzee Kobe aliamua kuwapa mtihani. aliwaambia, "Nendeni hadi kwenu mrudi kesho. Atakayewahi kurudi kesho ndiye atakayemuoa binti yangu.


Kesho yake, Kinyonga alienda na kujificha njiani. Sungura alichelewa, hivyo aliamua kwenda huku akitimua mbio. Alipokaribia kwa Mzee Kobe, Kinyonga alimdandia mkia bila Sungura kugundua. Sungura alipofika akataka kukaa, Kinyonga akamwambia usinikalie. Sungura akashtuka na akamuuliza Kinyonga, "Mbona ni mimi ndio nimeanza kufika?" Kinyonga akamjibu, "Mimi nimekuja asubuhi sana." Basi Mzee Kobe akamruhusu Kinyonga kumuoa binti yake kwa kuwa ilionekana kuwa Kobe ndiye aliyewahi kufika.

### Fundisho:

1.Hadithi hii hufundisha watoto kutowadharau wenzao kuwa hawawezi.

2.Ni muhimu kutumia akili kupata mafanikio.

3.Ni muhimu kubuni mbinu za kumshinda mshindani wako.



## 6 Uzuri Agundua Dawa ya Kuku

Hapo zamani za kale, katika kijiji cha Mitengwe, aliishi binti aitwaye Uzuri. Huyu alikuwa binti wa bwana Lisemwalo.

Wakati wa msimu wa joto hapo kijijini, Kuku waliugua sana. Walikuwa wakihara kinyesi cha njano. Hata kuku wa bwana Lisemwalo waliugua pia. Kuku wengi walitetemeka, kuvimba kichwa. Pia, walikuwa na madonda yenye upele vichwani mwao. Kuku wengi walidhoofu wakaacha kutaga mayai. Familia ya mzee Lisemwalo ilikosa mayai ya kuuza na kujipatia fedha za kukidhi mahitaji yao.

Siku moja Uzuri alimuona kuku mmoja akila ua la mshubiri. Baada ya siku mbili, yule Kuku alipona ugonjwa uliowapata kuku wengine wa Mzee Lisemwalo. Uzuri alifurahi sana. Alichuma ua la mshubiri na kulikatakata vipande vidogovidogo. Aliviloweka kwenye maji, kisha akawanywesha kuku wote. Kuku wote walipona na kuanza kutaga mayai tena. Uzuri alifurahi sana. Tangu siku hiyo, Uzuri akawa amegundua dawa ya kutibu magonjwa hatari ya kuku. Mzee Lisemwalo naye alifurahi sana na kumshukuru binti yake kwa ubunifu wake huo.

### Fundisho:

1.Fanya kazi za nyumbani kuwasaidia wazazi. 2. Shiriki kazi za nyumbani, utapata fursa ya kugundua vitu.

3.Kuwa mchunguzi na mbunifu kutatua changamoto katika familia.



## 7 Tuwalole Apika Wali Mtamu

Hapo zamani katika wilaya ya Kisarawe aliishi mzee mmoja aliyeitwa Shomvi. Alikuwa ameoa na alibahatika kupata mtoto mmoja tu aitwaye Tuwalole. Bwana Shomvi alikuwa mpishi hodari aliyejulikana kwenye vijiji vyote katika wilaya hiyo. Alikuwa akikodiwa kwenda kupika katika sherehe.

Tuwalole alikuwa ana miaka saba. Aliipenda sana kazi ya baba yake.

Siku moja mama yake Tuwalole aliondoka kwenda shambani. Baba yake naye aliaga kwenda kazini. Kabla ya kwenda kazini, alimwambia mtoto wake, "Tuwalole, kaa nyumbani. Usiondoke kwani mimi ninaenda kazini." Baadaye aliondoka kwenda kazini. Punde si punde, Tuwalole alifagia uwanja, na kumwagilia bustani ya mchicha na maua. Hatimaye, aliamua kujifunza kupika chakula. Alifanikiwa kupika wali mzuri kama baba yake! Mama yake aliporudi kutoka shambani, alishangaa kuona Tuwalole amepika wali mzuri sana. Aliuliza, "Baba yako amerudi na chakula kutoka kwenye sherehe leo?" Tuwalole alimjibu, "Hapana, nimekipika mimi kwa mikono yangu mwenyewe." Bwana Shomvi aliporejea nyumbani, mkewe alimsimulia namna Tuwalole alivyopika wali mzuri. Bwana Shomvi alifurahi sana, kisha alimwambia Tuwalole, "Utarithi kazi yangu." Tuwalole alimwambia, "Asante na ninaipenda kweli kazi yako. Nikiwa mkubwa lazima niwe mpishi hodari".

### Fundisho:

Hii hadithi inafundisha watoto kufanya kazi za nyumbani kuwasaidia wazazi na kujifunza stadi mbalimbali za maisha. Watoto wawe jasiri kujifunza mambo mazuri toka kwa wazazi kwa faida yao wenyewe.





Elimu Bora Tanzania inawezekana, Timiza wajibu wako!

Uwezo Tanzania
85K Suites Kinondoni Road | P .O. Box 8259 | Dar es Salaam | Tanzania
E: info@uwezotanzania.or.tz | Web: www.uwezotanzania.or.tz